أصول العقيدة - سواحيلي

# AQEEDAH YA MISINGI



جمعية الدعوة بالزلفي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

هاتف: ٤٢٣٤٤٦٦ ٠١٦ ـ فاكس: ٤٢٣٤٤٧٧ ٠١٦

# MISINGI YA AQEEDAH

## أصول العقيدة - سواحيلي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي
هاتف: 164234466 966 ـ فاكس: 164234477 966

# MISINGI YA AQEEDAH.

## أصول العقيدة

## TAUHEED NA AINA ZAKE.

Maana ya Tauheed.

Tauheed ni kumpwekesha Allah (sw) kwa yale ambayo ni khasa kwake yeye, ambayo ni wajibu katika aina za ibada, na hiyo tauheed ni katika jambo kubwa aliloliamrisha Allah (sw), Allah anasema katika quran:

قال الله تعالى: ﴿ قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ﴾ [الإخلاص:١]

("Sema yeye Allah ni mmoja tu") ( ikhlas : 1).

وقال سبحانه: ﴿ وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴾ [الذاريات: ٥٦]

Allah (sw) anasema: ("Sikuwaumba majini na binadamu isipokuwa ni kwa lengo la kuniabudu") (Adhariyat : 56).

وقال سبحانه: ﴿ وَاعْبُدُوا اللهَ وَلا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ﴾ [ النساء: ٣٦]

akaema tena Allah (sw) : ("Mwabuduni Allah wala msimshirikishe na chochote ") (Alnnisah: 36).

Tauheed imegawanyika vigawanyo vitatu (3) ;

1. Tauheed Rubuubiyah ( Ulezi wa Allah )
2. Tauheed Uluhiyyah ( Uungu wa Allah)
3. Tauheed Asmai wa swifat ( majina ya Allah na sifa zake)

## 1 : TAUHEED ALRUBUBIYYAH.

Maana yake ni kumpwekesha Allah (sw) katika kuumba, kuiendesha hii dunia, na kwamba yeye Allah ndiye mwenye kutoa riziki, mwenye kuhuyisha na kufisha, ndiye mwenye kumiliki mbingu saba na ardhi saba.

قال تعالى : ﴿ هَلْ مِنْ خَالِقٍ غَيْرُ اللهِ يَرْزُقُكُمْ مِنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ لا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَأَنَّى تُؤْفَكُونَ ﴾ [فاطر:٣]

Allah (sw) anasema : ("..... Hakuna muumba wenu zaidi ya mwenyezi mungu anaye awaruzuku nyinyi kwa mvua kutoka mbinguni, hapana mola isipokuwa yeye peke yake, basi vipi nyinyi mtaepushwa na kumpwekesha?") ( Fatir : 3 ).

وقال: ﴿ تَبَارَكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمُلْكُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴾ [ الملك: ١ ].

Allah anasema: ("Ametakasika yule ambaye mikonomi mwake upo ufalme wa duniani na Akhera, na yeye kwa kila jambo nimuweza") (Al-Mulk:1).

Na ufalme wake Allah (sw) ni ufalme uliokusanya kila kitu vilivyomo hapa duniani na kuviswarifu atakavyo. Ama kumpwekesha Allah (sw) katika kuendesha mambo yote Duniani ni kumpwekesha katika kuumba kwake.

قال سبحانه: ﴿ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ تَبَارَكَ اللهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴾[الأعراف:٥٤]

Anasema Allah (sw) (......" Uumbaji wote ni wake na ni yake yeye amri, ametukuka mwenyezi mungu bwana wa viumbe wote") (Al-a'raf:56).

Kuendesha mambo kuliko kamilika na kunakokusanya mambo ya viumbe wote.

Na hakuna waliokataa kuamini Tauheed hii isipokuwa kundi miongoni mwa wanaadamu, waliikataa hii tauheed wazi wazi, lakini nafsi zao zilikubali na kuikiri.

قال تعالى: ﴿ وَجَحَدُوا بِهَا وَاسْتَيْقَنَتْهَا أَنْفُسُهُمْ ظُلْمًا وَعُلُوًّا ﴾[النمل: ١٤]

Allah (sw) anasema : (" Na walikanusha Firauna na watu wake, na hali ya kuwa wana yakini ndani ya nyoyo zao, kwa kuifanyia uadui haki na kuwa na kiburi cha kutoikubali") ( An-naml : 14).

Kupwekesha peke yake hakumfai mtu, kama vile ambavyo hawakunufaika washirikina kwa kukiri kwao hii Tauheed Rububiyyah.

قال الله عنهم: ﴿ وَلَئِنْ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ لَيَقُولُنَّ اللهُ فَأَنَّى يُؤْفَكُونَ ﴾ [العنكبوت:٦١]

Allah (sw) anasema : ( " Ukiwauliza ewe Mtume hao washirikina, ni nani aliyeumba mbingu na ardhi kwa mpango huu mzuri na akalidhalilisha jua na mwezi, watasema ni alieviumba hivyo ni mwenyezi mungu peke yake, basi vipi wao watapotoshwa waache kumuamini mwenyezi mungu.") ( Al-ankabut:61).

## 2 : TAUHEED AL-ULUHIYYAH.

Maana yake ni kumpwekesha Allah (sw) katika aina zote za Ibada, kwamba asifanye mwanadamu na kuabudu pamoja na Allah (sw) kiumbe yeyote na kujikurubisha kwake huyo kiumbe.

Tauheed hii ndio tauheed muhimu sana kuifahamu, ndio tauheed ambayo Allah (sw) kawaumbia viumbe wote kwa ajili yake Allah (sw).

قال تعالى: ﴿ وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴾ [الذاريات:٥٦]

Allah (sw) anasema: ("Sikuwaumba majini na binadamu isipokuwa ni kwa lengo la kuniabudu") (Adhariyat: 56).

Tauheed hii ndio ambayo Allah (sw) aliwatuma mitume wake, akawateremshia na vitabu.

قال تعالى: ﴿وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ﴾ [الانبياء:٢٥].

Allah (sw) anasema: ("Hatukutuma Mtume wa aina yoyote kabla yako isipokuwa tulimfunulia ya kuwa hapana mola aabudiwaye kwa haki isipokuwa mimi (Allah) basi niabuduni") (Al-anbiyah: 25).
Tauheed hii ndio ambayo washirikina waliikataa na kuipinga wakati walipolinganiwa na mitume wa Allah (sw).

قال تعالى: ﴿ قَالُوا أَجِئْتَنَا لِنَعْبُدَ اللهَ وَحْدَهُ وَنَذَرَ مَا كَانَ يَعْبُدُ آبَاؤُنَا ﴾ [الأعراف:٧٠]

Allah (sw) anasema ("Wakasema kumwambia Hud, je umetuita tumuabudu mwenyezi mungu peke yake, na tuihame ibada ya masanamu ambayo tuliirithi kutoka kwa baba zetu") (Al –A'raf :70).
Haifai kufanya aina yoyote ya ibada kwa asiekuwa Allah (sw), sio kwa Malaika aliye karibu na Allah (sw), wala Nabii aliyetumwa, wala kwa Walii aliyekuwa mwema, wala yoyoye katika vumbe vyake Allah (sw),

kwani haifai ibada ya aina yoyote kufanywa asipokuwa ifanywe kwa ajili ya Allah (sw).

## 3 : TAUHEED AL-ASMAAI WASWIFAAT (MAJINA YAKE ALLAH NA SIFA ZAKE).

Maana yake ni kuamini majina yote ambayo Allah (sw) amejiita yeye mwenyewe na kujisifu kwayo, au aliyoitwa na kusifiwa na Mtume wake Muhammad صلى الله عليه وسلّم , na kuthibitisha hivyo katika hali ambayo inalingana na utukufu wake Allah (sw) bila ya kupindisha, wala kukataa ambacho ni wajibu kwake Allah, wala kumfananisha Allah na sifa ya viumbe, katika hali ya uhakika sio majazi, na kukanusha yale ambayo Allah (sw) yeye mwenyewe amekanusha na kukataa, au zile sifa ambazo Mtume wa Allah amezikanusha na kuzikataa, na zile ambazo hazijathibitishwa wala kukataliwa ni wajibu mtu kujiepusha nazo, haifai kuthibitisha wala kukanusha.

MIONGONI MWA MIFANO YA MAJINA YAKE ALLAH (SW).

Allah (sw) anayo majina mazuri aliyojiita yeye mwenyewe kama vile Allah yu hai na niwa tangu, kwa hiyo ni wajibu kwetu kuamini kuwa Allah yu hai, kwamba uhai ni miongoni wa sifa zake Allah (sw),

nayo ni uhai ulikamilika ambao haujatanguliwa na kukosekana uhai wala kuisha kuwa uhai wake umekoma.

Mwenyezi mungu amejiita kuwa ni mwenye kusikia (Assami'u), hapa ni wajibu juu yetu kuamini kuwa Allah (sw) kusikia ni sifa yake na ni jina miongoni mwa majina yake subhanahu wata'ala na kuwa Allah anasikia.

قوله تعالى: ﴿ وَقَالَتِ الْيَهُودُ يَدُ اللهِ مَغْلُولَةٌ غُلَّتْ أَيْدِيهِمْ وَلُعِنُوا بِمَا قَالُوا بَلْ يَدَاهُ مَبْسُوطَتَانِ يُنْفِقُ كَيْفَ يَشَاءُ ﴾ [المائدة:٦٤]

Miongoni mwa sifa za Allah (sw) anasema: ("Na mayahudi walisema, mkono wa mwenyezi mungu umefungwa kutotenda mema, mikono yao ndiyo iliyofungwa, na mwenyezi mungu amewafukuza kutoka kwenye rehema yake kwa sababu ya neno lao, bali mikono yake miwili imekunjuliwa, anatoa namna atakavyo") (Al- maidah: 63).

Anathibitisha Allah (sw) kwenye ayah hii kuwa anayo mikono miwili iliyosifika kwa ukunjufu wa kutoa zaidi kuwapa waja wake, kwa hiyo ni wajibu kuamini hivyo kuwa Allah (sw) anayo mikono miwili yenye kutoa iliyojaa neema mbali mbali, lakini ni lazima kuamini hivyo bila ya kujengea picha kwenye akili zetu, wala ndimi zetu kwa kutamka namna ilivyo hiyo mikono

miwili ya Allah (sw) na kuifananisha na mikono ya viumbe vyake.

قال تعالى: ﴿ لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴾ [الشورى:١١]

Allah (sw) anasema: ("Mwenyezi Mungu hana mfano wake na chochote, na yeye ni mwenye kusikia na kuona ") (Al-shurah: 11).

Ufupi wa maneno katika aina hii ya Tauheed, ni kwamba ni wajibu juu yetu kuyathibitisha yote aliyoyathibitisha Allah (sw) yeye mwenyewe, au yale aliyo thabitisha Mtume wake Muhammad (saw), na kuyakataa yale ambayo Allah mwenyewe ameyakaa au kukataliwa na Mtume wake Muhammad (saw) kutokana na majina yake Allah na sifa zake, bila ya kubadilisha, wala kufananisha au kupinga sifa miongoni mwa sifa zake Allah (sw) na kulinganisha.

## **MAANA YA KALIMAT TAUHEED** "LAAILAAHA ILLALLAH"

Kalimat "LAAILAAHA ILLALLAH" ndio msingi wa dini, neno hili lina nafasi kubwa sana katika dini ya kiislamu, kwani ndio nguzo ya kwanza katika nguzo za uislamu, pia ni sehemu katika sehemu za Imani, na kukubalika kwa matendo mema kwa kutamkwa

Laailaha Illallah, kujua maana yake na kufanyia kazi muktadha wake.
Ama maana ya haki ambayo haifaifahi kupindisha ni HAPANA MWENYE KUABUDIWA KWA HAKI ILA ALLAH, nayo ni kumpwekesha Allah peke yake katika Ibada, na kuacha Ibada isiyokuwa ya Allah (sw).
Miongoni mwa makosa ya kauli ni kwamba maana ya LAAILAAHA ILLALLAH, hapana muumba isipokuwa ni ALLAH, au hapana muweza au hapana alieanzisha isipokuwa ni Allah, au hakuna yeyote mwenye kupatikana isipokuwa ni Allah.

**NGUZO ZA KALIMAT LAAILAAHA ILLALLAH.**

Neno hili lina nguzo mbili ;

1. Nguzo ya kwanza ni kukataa.
2. Nguzo ya pili ni kukubali (Kuthibitisha).

Nguzo ya kwanza kukataa, ni kauli ya kusema "LAAILAAHA" nako ni kukataa uungu wa kila kitu hapa duniani.
Pili kukubali (kuthibitisha) ya kuwa hakuna mola isipokuwa ni Allah peke yake asiyekuwa na mshirika. Hakuna mola anayepaswa kuabudiwa isipokuwa Allah (sw), na wala haifai kufanya chochote katika aina za Ibada kwa asiyekuwa Allah (sw), kwani mwenye kulisema neno hili la LAAILAAHA ILLALLAH

akalijua maana yake, akaujua muktadhwa wake ya kuwa ni kujiepusha na shirki na kuthibitisha upweke wake Allah (sw) pamoja na kuitakidi kisawasawa ndani ya moyo wake, na kulifanyia kazi kwa mwenye kusema hayo, basi huyo atakuwa ni muislamu wa kweli.
Lakini mwenye kulifanyia kazi neno hili bila ya kuitakidi kwenye moyo wake, basi huyo atakuwa mnafiki, na mwenye kufanya kinyume ya hayo atakuwa mshirikina kafiri hata kama atalisema hili neno kwenye ulimi wake.

**UBORA WA KALIMAT TAUHEED** "LAAILAAHA ILLALLAH"

Neno hili "LAAILAAHA ILLALLAH" lina fadhila kubwa na faida nyingi, miongoni mwa fadhila zake ;

1. Neno hili ni sababu ya kumzuia mtu asikae milele motoni, kwa yule anaestahiki kuingia motoni miongoni mwa watu wa tauheed.

ففي الحديث أنَّ رسول الله - ﷺ - قال: (( يخرج من النار من قال: لا إله إلا الله، وفي قلبه وزنُ شعيرةٍ من خيرٍ ، ويخرج من النار من

قال: لا إله إلا الله ، وفي قلبه وزن بُرَّةٍ من خير، ويخرج من النار من قال: لا إله إلا الله ، وفي قلبه وزن ذَرة من خير )) [ متفق عليه: ٤٤ ، ١٩٣].

Katika Hadithi ya bwana Mtume (saw) anasema : ("Atatoka motoni yule mwenye kuitamka kalima ya LAAILAAHA ILLALLAH, na kwenye moyo wake ana uzito wa chembe ndogo ya kheri, atatoka motoni mwenye kusema LAAILAAHA ILLALLAH na kwenye moyo wake kuna punje ndogo ya kheri") ( Ameipokea Bukhar na Muslim).

2. Kwa ajili ya neno hili la tauheed, Allah (sw) amewaumba majini na wanadamu, Allah anasema :

قال الله تعالى: ﴿ وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴾ [الذاريات: ٥٦]

( " Sikuwaumba majini na wanadamu isipokuwa kwa lengo la kuniabudu") (al-Dhariyat:56). (yaani kunipwekesha)

3. Kwa neno hili Allah (sw) aliwatuma mitume wake na akateremsha vitabu kwa mitume.

قال تعالى: ﴿وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴾ [الانبياء:٢٥]

Allah (sw) anasema : (" Hatukutuma mtume yoyote kabla yako, isipokuwa tulimfunulia kwa kumpatia kitabu ya kwamba hakuna mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa mimi, basi niabuduni") (Al-Anbiyah:25).

4. Neno hili ndio ilikuwa ufunguo wa mitume kwenye Da'awa yao, ndilo neno la kwanza katika kulingania mitume, kila mtume alisema kuwaambia watu.

﴿... يَا قَوْمِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ﴾ [الأعراف:٥٩]

(" Enyi watu muabuduni Allah, hamna nyinyi mungu mwingine Zaidi yake yeye") (Al-A'araf:59).

## MASHARTI YA KALIMA YA LAAILAAHA ILLALLAH.

Kalima ya LAAILAAHA ILLALLAH inayo masharti saba, haifai mpaka yakusanyike masharti yote pamoja, na ashikamane nayo mtu bila ya kuacha hata sharti moja miongoni mwa masharti hayo ni;

1. Elimu (kujua) nayo maana yake ni kukataa na kuthibitisha nay ale yanayo lazimika kuyafanyia kazi, atakapo elewa mtu kuwa Allah (sw) ndiye anayestahiki kuabudiwa pekee, na kwamba ibada

yoyote ifanywayo kinyume ya Allah ni batili haifai, basi mtu huyo atakuwa ameifahamu maana halisi ya hili neno la LAAILAAHA ILLALLAH.

قال تعالى: ﴿ فَاعْلَمْ أَنَّهُ لا إِلَهَ إِلَّا اللهُ ﴾ [محمد: ١٩].

Allah (sw) anasema : ("Basi tambua na kujua ya kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni Allah peke yake") (Muhammad:19).

Hadithi ilipokelewa na Othman (Radhiyaaalahu Anhu), Mtume (saw) anasema :

وعن عثمان ﷺ، عن النبي -ﷺ- قال: (( من مات وهو يعلم أنه لا إله إلا الله دخل الجنة )) [ مسلم: ٢٦].

(" Yeyote atakaekufa hali yakuwa anajua ya kwamba hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah pekee ataingia peponi") (Amepokea Imamu Muslim).

2. Yakini , ni pale mtu kuitamka shahada kwa yakini iliyotulia moyoni mwake, bila ya kuingiwa na shaka inayowekwa na shetani wa kijini au wa kibinadamu, bali aiseme shahada akiwa na yakini ya kisawasawa.

قال الله تعالى: ﴿ إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا بِاللهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوا ﴾ [الحجرات: ١٥].

Allah (sw) anasema : (" Hakika si vinginevyya waumini wa kweli ni wale ambao wamemuamini mwenyezi mungu na mtume wake, kasha wakawa hawana shaka yoyote") (Al-hujrat :15).

وعن أبي هريرة - رضي الله عنه - أن رسول الله - صلى الله عليه وسلم - قال : (( أشهد أن لا إله إلا الله و أني رسول الله، لا يلقى الله بهما عبدٌ غيرَ شاكٍّ فيهما ، إلا دخل الجنة )) [ مسلم: ٢٧].

Hadithi aliyoipokea Abu Huraita Radhi za Allah ziwe juu yake, Mtume (saw) anasema: ("Mwenye kushuhudilia ya kuwa hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na akushuhudilia ya kwamba mimi ni mtume wa Allah, akawa mtu si mwenye shaka juu ya maneno mawili haya, isipokuwa ni kuingia peponi") (Ameipokea Imamu Muslim).

3. Kukubalika ni kuwa ukubali moyo na ulimi wake mtu kwamba kila ambacho kimeamuriwa na neno hili, basi asadikishe kwa kuelezwa, aamini kwa kila kilichokuja kutoka kwa Mtume (saw), na ayakubali hayo yote bila ya kuacha chochote kutoka kwake mtume (saw), Allah (sw) anasema:

قال الله تعالى : ﴿ آمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنْزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلٌّ آمَنَ بِالله وَمَلائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ لا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِنْ رُسُلِهِ وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ ﴾ [البقرة: ٢٨٥ ]

("Ameamini mtume wa mwenyezi mungu, yale aliyoletewa kwa njia ya wahyi kutoka kwa mola wake, na waumini pia wameamini, kila mmoja katika wao amemuaamini mwenyezi mungu ya kuwa ana malaika, ameteremsha vitabu na ametuma mitume, na hatukanushi yeyote katika mitume bali tunawaamini wote, na wanasema tumesikia na tumetii, tunatarajia msamaha wako mola wetu, na kwako pekee ndio marejeo") ( Al-Baqarah :285).

Na hayatakubaliwa kwa yule ambae atapinga baadhi ya hukumu za kisheria, kama vile kusimamisha hukumu ya haddi kwa wale ambao walioiba, kuzini, kupinga mtu kuoa wake Zaidi ya mmoja, kupinga mirathi ya kiislamu na mengi mengineyo ya kisharia.

قال تعالى: ﴿ وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ﴾ [الأحزاب:٣٦ ]

Allah (sw) anasema :("Haipaswi kwa muumini wa mwanaume wala muumini mwanamke, iwapo mwenyezi mungu na mtume wake wametoa uamuzi wataenda kinyume nao") (Al – Ahzab : 36).

4. Kufuata nako ni kujisalimisha, na huko kufuata ni lililojulishwa kwenye LAAILAAHA ILLALLAH, tofauti la Kufuata na kukubalika , ni kwamba kukubalika ni kudhihirika kwa jambo na kuswihi maana yake, ama kufuata na kufuatisha jambo kwa kufanya kwa vitendo.

Yeyote atakaejua maana ya LAAILAAHA ILLALLAH akayakinisha moyoni mwake, akaikubali lakini akaacha kuifuata, akaitangaza, akajisalimisha, akaufanyia kazi muktadha wa yale aliyoyajua kwenye hii kailma ya LAILAAHA ILLALLAH akawa wakati huo hajahakikisha sharti la kufuata, basi mtu huyo atakuwa na mapungufu kwenye kuifuata LAAILAAHA ILLALLAH.

قال الله تعالى: ﴿ وَأَنِيبُوا إِلَى رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ ﴾ [الزمر:٥٤]

Allah (sw) anasema ("...Na rejeeni kwa mola wenu na mjisalimishe kwake") (Az-zumar:53).

وقال تعالى: ﴿ فَلا وَرَبِّكَ لا يُؤْمِنُونَ حَتَّى يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لا يَجِدُوا فِي أَنْفُسِهِمْ حَرَجًا مِمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴾ [النساء:٦٥].

Allah (sw) anasema: ("Naapa kwa nafsi yake Allah tukufu, kwamba hawatamini kikweli mpaka wakufanye wewe ni hakimu kwenye ugomvi unaotokea baina yao, kasha wasiingiwe na dhiki

katika nafsi zao kwa matokea ya hukumu yako, na wajisalimishe kisawa sawa") (Ann- Nisaa:65).

5. Ukweli na huo ukweli ni mtu kusadikisha kwenye Imani yake, kusadikisha kwenye aqeeda yake kama ambavyo anasema Allah (sw) :

قال تعالى: ﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللهَ وَكُونُوا مَعَ الصَّادِقِينَ ﴾ [التوبة:١١٩]

(" Enyi mlioamini mcheni Allah na kuweni na watu wakweli") (At-Taubah :119).

Na mtume (saw) anasema :

وقال ﷺ: (( من شهد أن لا إله إلا الله صادقًا بها دخل الجنة )) [رواه أحمد ، وصححه الألباني]

("Mwenye Kushuhudia ya kwamba hakuna mola anayepaswa kubudiwa isipokuwa ni Allah, akawa ni mwenye kusadikisha LAILAAHA ILLALLAH ataingia peponi") (Ameipokea Imamu Ahmad na akaisahhihisha Al Bani).

Na atakapo itamka shahada kwa ulimi wake, akaikadhibisha kwenye moyo wake, basi haitamsaidia, bali ataingia na kuhesabiwa miongoni mwa watu wanafiki.

Miongoni mwa mambo yanayozuia ukweli ni kuyakadhibisha yale aliyokuja nayo bwana Mtume (saw) au kuyakadhibisha baadhi ya aliyokuja nayo mtume wa Allah, kwani Allah (sw) ametuamrisha kumtii mtume wake na kumsadikisha, akafungamanisha na kumtii yeye pale aliposema Allah (sw) :

قال تعالى: ﴿ قُلْ أَطِيعُوا اللهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ ﴾ [ النور:٥٤]

("mtiini Allah na mumtii Mtume ") ( An-Nur : 54).

6. Ikhlas nayo ni kutakasa mwanadamu matendo yake mema kwa nia njema , kutokana na chembechembe za kishirikina, kwa kufanya matendo yake yote ya maneno au ya vitendo yawe ni kwa ajili ya Allah (sw) na kutafuta radhi zake Allah, asiyafanye kwa kujionyesha kwa watu, au asemwe, au anafanya kwa kutaka manufaa fulani, au lengo maalumu, au anafanya kwa matamanio yaliyowazi au yaliyojificha, au anamkingia mtu kwa ajili ya mapenzi, madhehebu, kundi lisilokuwa kwenye muongozo wa Allah (sw), bali hapana budi yote atakayoyafanya ayafanye kwa kutafuta radhi zake Allah (sw) na malipo kesho Akhera, hatafuti kulipo na mtu yeyote wala kushukuriwa na mtu.

قال الله تعالى: ﴿ أَلَا لله الدِّينُ الخَالِصُ ﴾ [الزمر: ٣]

Allah (sw) anasema : (" Juwa na kutambua ya kuwa Allah peke yake ndie mwenye dini iliyotakasika") (Az-Zumar: 3).

وقال سبحانه: ﴿ وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ ﴾ [البينة: ٥]

Anasema Allah (sw) : (" Na hawakuamrishwa katika sharia zote zilizopita isipokuwa ni wamuabudu mwenyezi mungu peke yake, hali ya kutakasia yeye dini") (Al-Bayyinah:5).

Na imekuja kwenye sahihi mbili, bwana Mtume (saw) anasema :

وفي الصحيحين من حديث عِتبان قوله ﷺ: (( فإنَّ الله قد حَرَّم على النار من قال لا إله إلا الله ، يبتغي بذلك وجه الله )) [متفق عليه: ٤٢٥ ، ٣٣].

("Hakika ya Allah (sw) ameharamisha moto kuunguza mwenye kusema LAAILAHA ILLALLAH akitafuta radhi za Allah") (Ameipokea Bukhar na Muslim).

7. Kupenda، nako ni kuipenda LAAILAHA ILLALLAH na kila ambacho kinafungamana na hili neno, na ampende Allah na Mtume wake, na atangulize mapenzi ya kumpenda Allah na Mtume

wake kulikoni kitu chochote kile, ampende Allah mapenzi yanayo fungamana na utukufu wake Allah, na ukubwa wake Allah, na khofu yake Allah, na atarajie mema kutoka kwake Allah, na azipende sehemu zote anazozipenda Allah (sw) kama vile Makka, Madina na misikiti yote iliyopo duniani, na azipende zama kama vile mwezi wa Ramadhan, masiku kumi ya mwezi wa Dhul Hijja na masiku mwengine, na awapende viumbe watukufu kama vile Manabii, Mitume, Malaika wote, waja wema, Mashahidi, na pia apende matendo mema kama vile Swala, Zakat, Swaumu, Hijjah, na pia apende dhikri za kumtaja Allah na apende kusoma Quran.

Na miongoni mwa mapenzi kwa Allah ni kutakunguliza kila aina ya mapenzi kwake Allah kulikoni mapenzi ya nafsi yake mtu pamoja na matamaniwa yake.
Pia achukie kila ambacho Allah anakichukia, achukie ukafiri, ufasiki na uovu.
Allah (sw) anasema :

قال الله تعالى: ﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَنْ يَرْتَدَّ مِنْكُمْ عَنْ دِينِهِ فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهُ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ أَذِلَّةٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعِزَّةٍ عَلَى الْكَافِرِينَ يُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلا يَخَافُونَ لَوْمَةَ لائِمٍ ﴾ [المائدة:٥٤].

(“Enyi mlioamini, yoyote kati yenu atakayerudi nyuma akaiacha dini yake, basi Allah atawaleta watu bora kuliko wao, anao wapenda na wanompenda, mwenye huruma kwa waumini, wakali kwa makafiri, wanapigana jihadi na maadui wa mwenyezi mungu, na hawaogopi lawama za mwenye kulaumu”) (Al-maidah:54).

**MAANA YA KUSHUHUDIA KUWA MUHAMMAD NI MJUMBE WAKE ALLAH (SW).**

Maana yake ni kutambua kwa dhahiri na kwa ndani ya kwamba Muhammad (saw) ni mja wake Allah na mtume wake, amemtuma kwa ajili ya watu wote, na kwa kulifanyia kazi hili, ni kumtii mtume kwa yale yote anayo amrisha, na kumsadikisha yale anayo yaeleza na kujiepusha na yale yote anayoyakataza na kuyakemea na kusiabudiwe chochote ila kile ambacho kipo kwenye sharia ya Allah.

Na kushuhudia ya kuwa Muhammad ni Mtume wake Allah, kuna nguzo mbili muhimu ambazo ni;

- Nguzo ya kwanza ni Muhammad ni mja wa Allah na Mtume wake, nguzo hii inakataza kuchupa mipaka katika haki yake Mtume kuwa yeye ni mja wa Allah na mtume wake, na yeye Muhammad (saw) ni kiumbe aliyekamilika na hizi sifa mbili alizokuwa nazo.

Kwani maana ya kuwa ni mja wa Allah, kuwa yeye ni mja mwenye kumilikiwa, kwa hiyo ni mwanadamu aliyeumbwa miongoni mwa viumbe vyake Allah (sw), yanampata kama vile yanayo wapata wengine katika viumbe.

قال تعالى: ﴿ قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِثْلُكُمْ ... ﴾ [الكهف: ١١٠]

Allah (sw) anasema : (" Sema uwaambie kuwa, hakika sivinginevyo mimi ni mwanadamu mfano wenu") (Al- kahfi :110).

Allah (sw) anasema :

وقال سبحانه: ﴿ الحَمْدُ لله الَّذِي أَنْزَلَ عَلَى عَبْدِهِ الْكِتَابَ وَلَمْ يَجْعَلْ لَهُ عِوَجَا ﴾ [ الكهف: ١].

(" Kila sifa njema ni zake Allah ambae amemteremshia mja wake kitabu asikifanye ni chenye kupotoka") (Al-Kahf: 1).

- Nguzo ya pili ni kujua maana ya Rasuul (mjumbe wa Allah), maana yake ni aliyetumwa kwa watu wote kwa ajili ya kulingania kwa ajili ya Allah , kuwabashiria watu mambo ya kheri na kuwaonya watu na mambo ya shari, na katika kushuhudilia hili katika hizi sifa mbili ambazo ni kukataa kuchupa mipaka katika haki ya bwana mtume (saw), kwani

wako wengi katika wafuasi wake wanaochupa mipaka katika haki ya mtume na wakampandisha katika daraja ya juu Zaidi, kwa kumtoa katika nafasi yake yake ya utume na kumpandisha katika nafasi ya kuabudiwa kinyume ya Allah (sw), wakamtaka msaada kinyume ya Allah, wakamta awafanyie mambo asiyokuwa na uwezo nayo isipokuwa Allah pekee katika kuwakidhia haja zao, na kuwaondolea matatizo yao, na wako wengine ambao walipinga ujumbe aliokuja nao mtume (saw).

Wako ambao walimfuata mtume na kumtweza katika haki yake ya wajibu, wakayatanguliza maneno ya waja Zaidi kuliko maneno ya Mtume (saw), wakapuuza sunnah za mtume (saw) na wakategemea maneno yanayo kwenda kinyume na aliyokuja nayo mtume (saw).

# IMAANI YA NGUZO ZAKE.

## الإيمان وأركانه

**Imaan**:

Imaani ni maneno, vitendo na Itikadi.

Imaani inazidi kwa kuyafanya matendo mema ya kumtii Allah (sw), na inapungua imaani kwa kufanya matendo mabaya ya kumuasi Allah.
Nayo ni maneno yaliyomo moyoni na kutamkwa kwa ulimi, na matendo ya moyoni, kwa kutamka kwa ulimi na kafanya kazi viungo.
Kauli ya moyoni ni kuitakidi na kusadikisha moyoni, na kauli ya ulimi ni kukiri.
Na matendo ya moyo ni kujisalimisha, kujitakasa na kutangaza, kupenda, kufanya yaliyo mema.
Kufanya kazi viungo ni kuyafanya yaliyoamrishwa na kujiepusha na yaliyo katazwa.

Kwa hakika imewekwa wazi kwenye Quran na Sunnah za bwana Mtume (saw) ya kwamba Imaan ina nguzo zake, ambazo ni;
1: kumuamini Allah (sw)
2: Kuwamini malaika wa Allah.
3: Kuamini Vitabu vya Allah.

4: Kuwaamini Mitume wa Allah.
5: Kuamini siku ya mwisho.
6: Kuamini qadar ya Allah, kheri ni shari vyote ni vya Allah.

قال تعالى: ﴿ آمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنْزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلٌّ آمَنَ بِاللَّهِ وَمَلائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ لا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِنْ رُسُلِهِ وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ ﴾ [البقرة: ٢٨٥ ].

Allah (sw) anasema: ("Ameamini mtume wa mwenyezi mungu, yale aliyoletewa kwa njia ya wahyi kutoka kwa mola wake, na waumini pia wameamini, kila mmoja katika wao amemuaamini mwenyezi mungu ya kuwa ana malaika, ameteremsha vitabu na ametuma mitume, na hatukanushi yeyote katika mitume bali tunawaamini wote, na wanasema tumesikia na tumetii, tunatarajia msamaha wako mola wetu, na kwako pekee ndio marejeo") ( Al-Baqarah :285).

Na kama ilivyokuja katika sahihi Muslim kutokana na Hadithi ya Amir Muuminina Umar bin Khatwab (R.A) ya kwamba bwana Mtume (saw) anasema:

كما جاء في صحيح مسلم من حديث عمر بن الخطاب ﵁ : (أنَّ جبريل - عليه السلام - سأل النبي - ﷺ - عن الإيمان ، فقال له : (( الإيمان أن تؤمنَ بالله ، وملائكته ، وكتبه ، ورسله ، واليوم الآخر ، وتؤمن بالقدر خيره وشره )) [مسلم:٨].

("Hakika ya Jibir alayhi salaam alimuuliza mtume (saw) kuhusuana na Imaani, Mtume akamjibu akasema Imaan, ni kumuamini Allah, na Malaika wake, Kuamini vitabu vyake, kuamini Mitume wake, kuamini siku ya mwisho, na kuamini qadar kheri na shari") (Ameipokea Imamu Muslim).

Kwa haya mambo sita, ndio misingi mikuu ya Aqeeda sahihi ambayo iliteremka kwenye kitabu cha Allah (Quran), na ndiyo ambayo alitumilizwa kwayo bwana Mtume (saw) na ndio inayoitwa NGUZO ZA IMAAN.

## 1 : NGUZO YA KWANZA YA IMAAN NI KUMUAMINI ALLAH (SW).

Nayo ni kumpwekesha Allah (sw) katika uungu wake, ulezi wake, na majina yake na sifa zake.

Miongoni mwa kumuamini Allah (sw) ni;

1 : Ni kuamini kuwa Allah ndiye mwenye kustahiki ibada peke yake, kwa kuwa yeye ndiye muumba wa

viumbe wote, aliye wafanyia ihsani, anae wasimamia riziki zake, na anayejua siri zao na dhahiri zao, mwenye uwezo wa kuwalipa thawabu wenye kumtii na kuwaadhibu wenye kumuasi.

Na uhakika wa hilo ni kuwa Imaani ni kumpwekesha Allah katika yote anastahiki kuabudiwa katika aina zote za ibada, katika hali ya unyenyekevu, katika kupenda na kuwa na hofu juu ya Allah (sw), pamoja na mapenzi ya dhati kwa Allah (sw) na kujidhalilisha katika utukufu wake Allah subhanahu wataalah.

Mwenyezi mungu anasema kuhusu msingi mkubwa ulioshuka Quran Allah (sw) anasema:

قال تعالى: ﴿ فَاعْبُدِ اللهَ مُخْلِصًا لَهُ الدِّينَ. أَلا للهِ الدِّينُ الخَالِصُ ﴾

[الزمر:٢-٣]

("Muabudu mola wako kwa kumtakasia yeye dini, zindukeni hakika mwenyezi mungu ndie mwenye dini iliyotakasika") (Az- zumar: 2-3).

وقوله: ﴿ وَقَضَى رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ ﴾ [الاسراء:٢٣]

Allah (aw) anasema : (" Amehukumu mola wako ya kuwa msiabudu chochote idipokuwa yeye tu peke yake..") (Al-Israh : 23).

Zipo aina nyingi za ibada miongoni mwa ibada hizo ni; Kuomba dua, kuwa na khofu, kuwa raja, kumtegemea Allah, kuwa na raghaba na uoga, kunyenyekea, kuogopa, kurejea kwa Allah, kutaka msaada, kujikinga, kuchinja, kuweka ndhiri, na nyinginezo katika aina za ibada ambazo haifai kuzifanya ibada hizi na nyingine kunyume na Allah (sw), na atakaefanya ibada miongoni mwa ibada hizi kwa asiekuwa Allah atakuwa amemshirikisha Allah (sw) na kukufuru.

Ushahidi wa dalili ya kuwa Dua ni ibada Allah (sw) anasema:

قوله تعالى: ﴿ وَقَالَ رَبُّكُمُ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ﴾ [غافر:٦٠]

("Amesema mola wenu niombeni nitazijibu dua zenu, hakika wale ambao wanafanya kiburi cha kutoniomba, wataingia moto wa jahanaba hali ya kuwa ni wadhalilifu") (Ghafir : 60).

وفي الحديث ما رواه النعمان بن بشير رضي الله عنه، عن النبي - ﷺ - أنَّه قال: (( الدُّعَاءُ هوَ العِبَادَةَ )) [رواه الترمذي: ٢٩٦٩].

Na hadithi aliyoipokea Nu'uman bin Bashir (R.A) kutoka kwa Mtume (saw) anasema: ("Dua ndio Ibada") (Ameipokea Tirmidhiy).

قال تعالى: ﴿ فَلاَ تَخَافُوهُمْ وَخَافُونِ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴾ [آل عمران:١٧٥].

Dalili ya ghofu ni kauli yake Allah aliposema: ("Msiwaogope hao nigopeni mimi, ikiwa nyinyi ni waumini") (Al- Imran :175).

Dalili ya kutarajia kukutana na Allah ni neno lake Allah (sw) aliposema:

قال تعالى: ﴿ فَمَن كَانَ يَرْجُو لِقَاء رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلاً صَالِحاً وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدًا ﴾ [الكهف:١١٠].

("Basi yeyote anayetarajia kukutana na mwenyezi mungu, basi afanye matendo mema na asimshirikishe Allah kwenye ibada yake na yeyote") (Al-Kahf: 110).

Dalili ya kutawakkal, Allah (sw) anasema:

قال تعالى: ﴿ وَعَلَى اللهِ فَتَوَكَّلُواْ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ﴾ [المائدة: ٢٣]

("Na kwa mwenyezi mungu mtegemeeni ikiwa nyinyi ni waumini") (al-maidah:23).

وقوله: ﴿ وَمَن يَتَوَكَّلْ عَلَى اللهِ فَهُوَ حَسْبُهُ ﴾ [الطلاق:٣].

Anasema tena Allah : (" Na yeyote atakae mtegemea mwenyezi mungu basi yeye atamtosheleza") (At-Talaq: 3).

Dalili ya raghaba (matumaini ya kupata mazuri) na Rahbah (khofu/ kuogopa), Khushuu (unyenyekevu) Allah (sw) anasema:

قال تعالى: ﴿ إِنَّهُمْ كَانُوا يُسَارِعُونَ فِي الخَيْرَاتِ وَيَدْعُونَنَا رَغَبًا وَرَهَبًا وَكَانُوا لنَا خَاشِعِينَ ﴾ [الأنبياء:٩٠].

("Kwa kweli wao walikuwa wakiikimbilia kila kheri wakitumai kupata mazuri yaliyopo kwetu wakiogopa mateso yetu na walikuwa wadhalilifu na wanyonge kwetu") (Al-Anbiya: 90).

Dalili ya khashiya (kuogopa) Allah anasema:

قوله تعالى: ﴿ فَلاَ تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِي ﴾ [البقرة:١٥٠].

("Basi msiwaogope niogopeni mimi") (Al-Baqara: 150).

Na dalili ya kurejea kwa Allah ni:

قوله تعالى: ﴿ وَأَنِيبُوا إِلَى رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ ﴾ [الزمر:٥٤].

("Na rejeeni kwa mola wenu enyi watu, kwa kutii na kutubia na mnyenyekeeni...) (Az-Zumar:54).

Na dalili ya kuomba msaada kwa Allah:

قوله تعالى: ﴿ إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴾ [الفاتحة:٥]

("Kwako wewe tu tunakuabudu na kwako wewe tu tunakuomba msaada") (Al-Fatihah:5).

وقوله ﷺ : (( إِذَا اسْتَعَنْتَ فَاسْتَعِنْ بِاللهِ )) [رواه الترمذي: ٢٥١٦]

Na anasema Mtume (saw) : (" Unapotaka kuomba msaada basi taka msaada kwa Allah") (Ameipokea Tirmidhiy 2516).

Dalili ya kujikinga kwa Allah :

قَوْلُهُ تَعَالَى: ﴿ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴾ [الناس:١].

(" Sema ewe Muhammad najikinga kwa mola wa watu") (an-Nas:1).

Dalili ya kuomba kupata msaada (istighaathat) allah anasema :

قوله تعالى: ﴿ إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ لَكُمْ ﴾ [الأنفال:٩].

("Mkumbukeni mola wenu wakati mlipoomba mwenyezi mungu mpate ushindi kwa maadui wenu, mwenyezi mungu akakubali maombi yenu...") (Al-Anfal:9).

Dalili ya kuchinja, mwenyezi mungu anasema:

قوله تعالى : ﴿ قُلْ إِنَّ صَلاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ لاَ شَرِيكَ لَهُ وَبِذَلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَاْ أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ ﴾ [الأنعام:١٦٣].

("Sema ewe Mtume, hakika swala yangu, na kuchinja kwangu na uhai wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya mwenyezi mungu mola wa vioumbe wote. Asie na mshirika katika uungu wake, huko ndiko niliko amrishwa na mimi ni wa kwanza kumfuata mwenyezi mungu") (Al- An'am:162).

Na miongoni mwa dalili za sunnah ya mtume katika kuchinja ni ;

قوله ﷺ: (( لَعَنَ اللهُ مَنْ ذَبَحَ لِغَيْرِ اللهِ )) [رواه مسلم: ١٩٧٨].

("Mwenyezi mungu amemlani mwenye kuchinja kinyume ya Allah ") (Ameipokea Imam Muslim).

Na dalili kuweka nadhiri Allah anasema:

قوله تعالى: ﴿ يُوفُونَ بِالنَّذْرِ وَيَخَافُونَ يَوْمًا كَانَ شَرُّهُ مُسْتَطِيرًا ﴾

[الإنسان:٧].

("wanatekeleza nadhiri walizoziweka, na wakiogopa ya kiyama ambayo madhara yake ni hatari na ubaya wake ni wenye kusambaa na kuenea kwa watu") (Al-Insan:7).

Iwapo mazowea pindi yatakapo kusudiwa ucha mungu na kumtii mwenyezi mungu kama vile kulala, kula, kunywa, kutafuta riziki, kuoa na mengineyo, mazoea hayo akayafanya kwa nia njema basi itakuwa ni ibada na atalipwa muislamu ujira na thawabu juu yake.

2: Miongoni mwa kumuamini Allah, ni kuamini yote aliyoyawajibisha na kuyalazimisha mwenyezi mungu kufanywa katika ibada zake na akafaradhisha juu ya waja wake katika nguzo tano za Uislamu za dhahiri ambazo ni kutoa shahada ya kwamba hapana mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kushuhudia ya kuwa Muhammad ni mjumbe wake Allah na Mtume wake, na kusimamisha swala tano, na kutoa zakat, na kufunga mwezi wa Ramadhan na kwenda kuizuru nyumba tukufu ya makkah (Al-Ka'aba) kwa mwenye uwezo wa kwenda huko.
Pamoja na kutekeleza faradhi nyingine zilizokuja kwenye sharia tukufu ya Allah.

3: Na katika kumuamini mwenyezi mungu, ni kuamini ya kuwa mwenyezi mungu ndiye alieumba ulimwengu na kuyaendesha mambo ya walimwengu

wote kwa ujuzi wake Allah na uwezo wake atakavyo yeye, na kwamba yeye ndiye mmiliki wa dunia na akhera, mlezi wa viumbe wote, hakuna muumbaji zaidi yake, hakun mola mlezi zaidi yake, yeye ndiye aliwatuma mitume wote, ameteremsha vitabu kwa lengo la kuwafanyia islahi waja wake kwa kuwalingania kwenye mambo ambayo kwao yana masilahi ya kufaulu duniani na akhera.

Kwa hayo yote mwenyezi mungu hana mshirika, kama alivyosema kuwa

قال تعالى: ﴿ اللَّهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ ﴾ [الزمر: ٦٢]

(" Mwenyezi mungu ndiye muumba wa vitu vyote, na ni mtunzi wa kila kitu") (Az-Zumar: 62).

4: Katika Imaani ya Kumuamini mwenyezi mungu, ni kuyaamini majina yake mazuri na sifa zake zilizo tukuka, zilizoelezwa katika kitabu chake kitukufu ambacho ni Quran na kuthibitishwa na Mtume wake muaminifu Muhammad (saw) bila ya kupindisha wala kuacha sifa yoyote, wala kubadilisha wala kufananisha na sifa ya kiumbe yeyote.

Pamoja na kuamini yale yenye maana tukufu kuwa ni miongoni mwa sifa zake Allah (sw) ambazo ni wajibu kusifiwa kwa kuendana naye zisizofanana na sifa za

kiumbe yeyote aliye muumba, kama anavyosema Allah (sw) :

قال تعالى: ﴿ لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴾ [الشورى:١١].

("Hana mfano na chochote mwenyezi mungu, nay eye anasikia na kuona") (Ashurah:11).

## 2 : NGUZO YA PILI NI KUAMINI MALAIKA WA ALLAH.

Inakusanya nguzo hii kuwaamini malaika wote kwa pamoja na kuamini Malaika hawa kwa ufafanuzi zaidi.

Ama kuamini malaika wote kwa pamoja, ni kuamini ya kwamba mwenye zi mungu anao malaika aliowaumba kwa ajili ya kumtii yeye, na hao malaika wako aina nyingi, miongoni mwao ni;

- Malaika wanaobeba A'arsh ya Allah
- Malaika wa peponi na motoni
- Malaika waliowakilishwa kwa kuhifadhi matendo ya waja wake allah.

Ama katika njia ya ufafanuzi, tunaamini ya kuwa wale aliowaita majina yao Allah na Mtume wake kama vile Malaika Jibril, Mikail, na Malaika Mwenye kumiliki khazina za Motoni, Israfil aliye wakilishwa katika kupuliza parapanda.

Na malaika hawa Allah amewaumba kwa nuru kama ilivyothibiti kutoka katika Hadithi ya mama Aisha mkewe Mtume Muhammad (saw) aliyoipokea Imamu Muslim, Mtume (saw) anasema :

كما ثبت عن عائشة - رضي الله عنها - أنَّ النبي - ﷺ - قال: (( خُلقت الملائكة من نور ، وخُلق الجان من مارج من نار ، وخُلق آدم مما وُصِفَ لكم ))

[رواه مسلم: ٢٩٩٦].

("Wameumbwa Malaika kwa Nuru na wameumbwa Majini kutokana na ndimi za moto na ameumbwa Adam kutoka na yale mliyoelezewa").

## 3 : NGUZO YA TATU NI KUAMINI VITABU VYA ALLAH.

Ni wajibu kuamini moja kwa moja ya kuwa mwenyezi mungu ameteremsha vitabu kwa manabii wake na mitume wake ili kubainisha haki kwa waja wake na kulingani kwa kutumia hivyo vitabu.

Tuamiani katika njia ya ufafanuzi kwa yale aliyoyasema mwenyezi mungu, miongoni mwa vitabu hivyo ni Taurat, Injili, Zabur na Quran, na Quran ndio kitsbu cha mwisho kuteremshwa, kimekuja kulia nguvu na kuvisadikisha vitabu vilivyo tangulia'

Kwa hiyo ni wajibu kwa watu wote kuifuata Quran na kuitolea hukumu katika mambo yao yote na kutumia yale yote yaliyo kuwa sahihi katika mafundisho ya Mtume Muhammad (saw), kwani mwenyezi mungu amemtumiliza Muhammad mtume kwa viumbe wa aina mbili (Athaqalaini- Majini na Binadamu) na akateremshiwa hii Quran ili awahukumu baina yao.
Mwenyezi mungu akaifanya Quran kuwa ni pozo (dawa) kwa yale yote yaliyomo vifuani mwa waja na niufafanuzi wa kila kitu, na ni muongozo na ni rahma kwa watu wote, Allah anasema:

قال تعالى: ﴿ وَهَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ فَاتَّبِعُوهُ وَاتَّقُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴾ [الأنعام:١٥٥]

("Na hiki kitabu tumekiteremsha kimebarikiwa, basi kifuateni na mcheni mwenyezi mungu ili mpate kurehemewa ") (Al – Ani'am:155).

Allah anasema:

وقال سبحانه: ﴿ وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تِبْيَاناً لِكُلِّ شَيْءٍ وَهُدىً وَرَحْمَةً وَبُشْرَى لِلْمُسْلِمِينَ ﴾ [النحل:٨٩]

("Tumekuteremshia kitabu uwe ni upambanuzi wa kila jambo na ni muongozo na ni rahma na bishara njema kwa waislamu") (An-nahl: 89).

## 4: NGUZO YA NNE YA IMAANI NUKUAMINI MITUME WA ALLAH.

Ni wajibu kuwaamini Mitume wote kwa pamoja na kwa kupambanuzi, tuamini ya kwamba Allah (sw) amewatuma Mitume kwa waja wake, kwani Mitume ni wenye kubashiria watu mambo mema na kuwaonya watu na mambo maovu wao ni walinganiaji kwenye haki.
Allah (sw) anasema :

قال تعالى: ﴿ وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولاً أَنِ اعْبُدُوا اللهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ ... ﴾ [النحل:٣٦]

("Kwa hakika tulituma kwa kila umma mtume, kuwaambia watu wake wamuabudu mwenyezi mungu na wajiepushe na twaghuti") ( An-Nahl:36).

Mwenye kuitikia wito wa Mitume atafaulu na kusalimika, na mwenye kupinga wito wao ataa ngamia na kujuta.

Tunaamini kuwa ulinganiaji wa Mitume wote ni mmoja, nao ni ulinganiaji wa kumpwekesha mwenyezi mungu katika ibada, lakini waliitalafiana kwenye hukumu na sharia zao walizopewa na mwenyezi mungu.

Tunaamini kuwa wako Mitume bora kati yao, na mbora wao kati ya hao wote ni Mtume wa mwisho Muhammad (saw).
Allah (sw) anasema :

قال سبحانه: ﴿ وَلَقَدْ فَضَّلْنَا بَعْضَ النَّبِيِّينَ عَلَى بَعْضٍ ﴾ [الاسراء:٥٥]

("Na kwa hakika tumewafadhilisha baadhi ya Mitume juu ya wengine") ( Al Israh: 55).

وقال سبحانه: ﴿ مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِنْ رِجَالِكُمْ وَلَكِنْ رَسُولَ اللهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ ﴾ [الأحزاب:٤٠].

Allah (sw) anasema : (" hakuwa Muhammad ni baba wa mmoja katika waume zenu , lakini ni Mtume wa Mwenyezi mungu na ni mwisho wa Mitume") ( Al-Ahzab:40).

Na wale ambao Allah amewataja miongoni mwao au akathibitisha mtume wake majina yao, tunawaamini kwa ufafanuzi na kuelezwa kama vile mtume Nuhu, Hud, Swaleh, Ibrahim na wengineo pamoja na mbora wa Mitume Muhammad (saw).

## 5 : NGUZO YA TANO KUAMINI SIKU YA MWISHO.

Nguzo hii inaingia ndani yake kila ambacho Allah amekieleza yeye na mtume wake (saw), katika yale ambayo yatakuwa baada ya kufa na fitna za kaburi, adhabu za kaburi na neema za kaburi, n yale yatayotokea siku ya kiyama kutoka na vituko vyake na shida za siku hiyo. Na kupita kwenye Swiratwa (njia Maalum), Mizani, Hisabu na malipo, na kugawiwa watu vitabu vya matendo yao baina ya watu, yupo atakae chukua kitabu chake kwa mkono wa kulia, na mwengine atachukua kitabu chake kwa mkono wa kushoto kwa kutokea nyuma ya mgongo.
Kwenye nguzo hii pia kunaingia Imaani ya kuamini kuwa kuna birika (Haudhwi) aliloandaliwa kunywa maji yake Mtume wetu Muhammad (saw), kwani kila Mtume analo birika lake, kama ilivyokuja katika hadithi za mtume (saw), pia katika nguzo hii inaingia Imaani ya kuamini pepo na moto, waumini kumuona Mola wao siku ya Kiyama na kuwasemesha na mengineyo kama ilivyokuja kwenye Quran na Sunnah za Mtume (saw), ni wajibu kuyaamini hayo yote na kuyasadiki katika hali ambayo ameibainisha mwenyezi mungu na Mtume wake.

## 6 : NGUZO YA SITA NI QADAR.

Na katika nguzo hii kuna kusanyika mambo makuu manne;
1: Jambo la kwanza: Mwenyezi mungu anayajua yaliyotangulia na yatakayokuwa baadae, anazijua hali za waja wake kanzia riziki zao, ajali zao, matendo yao na mengineyo katika mambo yao hakuna kilichojificha kwake Allah (sw).
Allah (sw) anasema:

قال سبحانه: ﴿ إِنَّ اللهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴾ [التوبة:١١٥].

("Hakika ya mwenyezi Mungu juu ya kila kitu ni mjuzi") (At-Tawbah:115).

2: Jambo la Pili : Kuamini kuwa kila alicho kiandika mwenyezi mungu amekikadiria na kukidhibiti hukumu yake.

Allah anasema :

قال سبحانه: ﴿ وَكُلَّ شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ فِي إِمَامٍ مُبِينٍ ﴾ [يس:١٢].

(" Hakika kila kitu tumekidhibiti katka kitabu chenye ufafanuzi") (Yasin : 12).

3 : Jambo la Tatu : Kuamini Matakwa yake Allah (Mashiatun) yaliyotekelezwa tokea zamani, alitakalo mwenyezi mungu linakuwa na asilolitaka haliwi.
Allah anasema :

قال سبحانه: ﴿ كَذَٰلِكَ اللهُ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ ﴾ [آل عمران:٤٠].

("Hivyo basi Mwenyezi Mungu anafanya atakavyo") (Al Imran: 40).
4 : Jambo la Nne : Kuamini ya kuwa Mwenyezi mungu ndiye aliyaumba yaliyo kadiriwa kabla ya kutokea.

Allah anasema :
قال سبحانه: ﴿ وَاللهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ﴾ [الصافات:٩٦].

(" Na Mwenyezi Mungu ndiye aliye waumbeni nyinyi na yale mnayoyatenda") (As-swafat: 96).

# SHIRKI NA AINA ZAKE

## الشرك وأنواعه

SHIRKI ni mja kumfanyia Mwenyezi mungu kuwa kuna mungu mwingine kinyume ya Allah katika ulezi wake, uungu wake na katika majina yake na sifa zake.

SHIRKI ZIKO AINA MBILI :

- Shirki kubwa
- Shirki ndogo

**SHIRKI KUBWA**.

Shirki kubwa ni kufanya aina yeyote ya ibada kinyume na Allah (sw), na mwenye kufanya shirki atakaa motoni milele ikiwa atakufa bila ya kutubia kwa Allah.

Shirki inabatilisha matendo mema ya mtu, Allah anasema :

قال تعالى: ﴿ وَلَوْ أَشْرَكُوا لَحَبِطَ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ﴾ [الأنعام: ٨٨]

("Na lau kama watamshirikisha mwenyezi mungu, basi yatapomoka yote waliyokuwa wakiyafanya") ( Al-Anam: 88).

Na shirki kubwa mwenyezi mungu haisamehe isipokuwa mtu mpaka atubie toba ya kisawaswa.

قال تعالى: ﴿ إِنَّ اللهَ لا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ وَمَنْ يُشْرِكْ بِالله فَقَدِ افْتَرَى إِثْماً عَظِيمًا ﴾ [النساء:٤٨].

Allah anasema: ("Hakika ya Allah hasamehe dhambi ya kushirikishwa, na anayasamehe madhambi mengine yasiyokuwa shirki, na mwenye kumshirikisha mwenyezi mungu kwa hakika amezua dhambi kubwa sana") (An-nisah: 48).

Miongoni mwa aina za kubwa ni kuomba kwa asiyekuwa mwenyezi mungu, au kuweka nadhiri kwa asiyekuwa mwenyezi mungu, au kuchinja kwa asiyekuwa mwenyezi mungu, na vinginevyo, au kufanya kwa asiyekuwa mwenyezi mungu miungu mingine na kuipenda zaidi ya Allah (sw).

قال تعالى: ﴿ وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَتَّخِذُ مِنْ دُونِ الله أَنْدَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ الله ﴾ [البقرة:١٦٥] .

(Wako miongoni mwa watu wanachukua badala ya mwenyezi mungu miungu mingine, wakiwapa mapenzi kama wanavyo mpenda mwenyezi mungu) (A-Baqarah:165).

**AINA YA PILI YA SHIRKI NI SHIRKI NDOGO.**

Shirki ndogo ni ile ambayo imeelezwa kwenye quran au hadithi za Mtume Muhammad (saw) akaisema kuwa ni shirki lakini ikawa haijafika kiwango cha shirki kubwa.

Shirki hii ndogo haimtoi mtu katika uislamu tofauti na shirki kubwa, lakini inapunguza kupwekesha Allah, kama vile mtu kuwa na Riya, na kauli ya kusema ametaka mwenyezi mungu na wewe, na kusema lau sikama mwenyezi mungu na wewe, pia kuapa kwa asiyekuwa mungu, bila ya kuitakidi kuwa kinachoapiwa kinanufaisha au kinadhuru kinyume ya mwenyezi mungu.

Pia kusema kuwa akitaka mwenyezi mungu na kutaka Fulani basi jambo hili lingekuwa hivi hivi n.k.

لقول النبي ﷺ: ((أَخوفُ ما أَخافُ عليكم الشرك الأصغر))، فسُئل عنه، فقال: (( الرياء )) [رواه أحمد وإسناده جيد]

Mtume (saw) anasema : ( Kitu cha kuwahofisha zaidi juu yenu ni Shirki ndogo, akaulizwa Mtume ni ipi hiyo? Mtume akasema ni Mtu kuwa na Riya) (Ameipokea Imamu Ahmad na Mapokezi yake ni mazuri).

وقوله ﷺ : (( منْ حَلفَ بغير الله فقد أشرك )) [رواه أبو داود: ٢٨٢٩] .

Mtume (saw) anasema : (Mwenye kuapa kinyume ya mwenyezi mungu, kwa hakika amefanya shirki) (Amaipokea Imam Abu Daud : 2829).

Matendo yanayofungamana na shirki ndogo ni kufunga Hirizi, kufunga bangili au uzi kwa lengo la kukuondolea madhara au kukukinga na maradhi pamoja na matatizo, lakini mtu akaitakidi kuwa inanufaisha au kudhuru na kwamba sio sababu ya kudhurika au kunufaika, basi hiyo itaingia kwenye shirki kubwa.

# ITIKADI YA KUNDI LILILO FAULU.

## مجمل اعتقاد الفرقة الناجية

Itikadi ya kundi lililofaulu ndio itikadi ya Ahlu sunnah waljamaa, nayo ni itikadi ya kuamini haki, kushuhudia ya kuwa Allah peke yake ndiye anaestahiki kuabudiwa, aliyepweke kwa ukamilifu, mwenye kuabudiwa na kutakasiwa yeye pekee dini, na kuelewa ya kuwa Allah pekee ndiye muumbaji, muanzilishi wa uumbaji, anayewapa sura viumbe wake kulingana na hekma yake, mwenye kutoa riziki, mwenye sifa ya kutoa, mwenye sifa ya kuzuia, mwenye sifa ya kuendesha mambo yote ya viumbe wake.

Na hakika yeye mwenyezi mungu ndiye anaestahiki kuabudiwa kwa haki, nay eye ndie wa mwanzo hakuna bala yake chochote, yeye ndie wa mwisho hakuna baada yake chochote, yeye yupo hakuna juu yake chochote, na yeye amejificha hakuna chini yake chochote.

Na kwamba mwenyezi mungu yupo juu ya kila kitu, hakuna juu yake chochote zaidi yake, kwa maana yake halisi na mazingatio, Allah yupo juu kwa dhati yake, uwezo wake na nguvu zake.

Na kwa hakika Allah yupo juu ya A'arshi yake ametulia, kulia kunako lingana na utukufu na ukubwa wake Allah, ujuzi wake Allah umeenea kila kitu dhahiri na ndani, mwenyezi mungu ni mjuzi wa kujua yaliyo juu na chini, anawajua waja wake vizuri, anazijua hali zao zote, na yeye yupo karibu kujibu dua zao wanapo muomba.

Hakika ya mwenyezi mungu ni mkwasi ametosheka kwa viumbe vyake vyote, na viumbe vyote kwake ni masikini vimeumbwa na vyote wanavyo hitajia nyakati zote pia vimeumbwa.

Hakuna chochote chenye kujitosheleza hata kiasi cha kupepesa jicho na yeye mwenyezi mungu ni mpole mwenye huruma, ambaye hakuna kwa waja wake neema ya aina yoyote ya dini wala ya dunia isipokuwa inatoka kwake yeye na yeye ndie mwenye kuleta hizo neema na ndie anaeondoa na kukinga mabalaa.

Kutokana na huruma zake mwenyezi mungu, anateremka kuja mbingu ya dunia wakati ikibaki thuluthi ya mwisho ya usiku.

فيقول: ((مَنْ ذا الذي يسألني فأُعْطِيَه، من ذا الذي يستغفرني فأغفرَ له)) حتى يطلع الفجر، فهو ينزل نزولًا يليق به جل شأنه.

(Ni nani mwenye kuniomba nimpe, ni nani mwenye kunitaka msamaha nikamsamehe, hali hiyo mpaka kuchomoza kwa alfajir, na kuteremka kwake mwenyezi mungu kunalingana na utukufu wake mwenyezi mungu).

Mwenyezi mungu ni mwingi wa hikma iliyopea katika sharia zake na qadari yake, hakuumba chochote bure wala hakuweka sheria isipokuwa kwa maslahi ya waja wake na kuepusha na mabaya.

Mwenyezi mungu ni mwingi wa kukubali toba na kusamehe, anakubali toba za waja wake na anasemehe makosa, anasamehe makosa makubwa kwa mwenye kutubia na kurejea kwake.

Na mwenyezi mungu ni mwenye kushukuru, anashukuru kidogo katika matendo ya mja, na anamlipa malipo makubwa na mengi, na anawazidishia zaidi kwa wale wenye kumshukuru kutokana na fadhila zake.

Muumini wa kweli anaelezea sifa za Allah vile alivyo jisifu mwenyewe na alivyo sifiwa na mtume wake katika sifa za dhati yake na sifa za vitendo, kama vile sifa ya uhai iliyo kamili, sifa ya kusikia na kuona, sifa ya ukamilifu wa uwezo, utukufu na kibri, sifa ya utukufu, uzuri na ukamilifu pamoja na sifa zote nzuri zinazo mstahiki yeye Allah.

Muumini aamini yote yaliyokuja kwenye kitabu cha Allah na kufuatiliwa na sunnah za bwana mtume Muhammad (saw), kwa kuwa waumini watamuona mola wao siku ya kiyama peponi kwa macho ya wazi kabisa, ni neema kumuona mwenyezi mungu, na kufaulu kwa kupata radhi zake ni neema kubwa zaidi na ladha kubwa ya peponi.

Na yeyote mweye kufa bila ya kuwa na Imaani na Tauheed, basi mtu huyo atakaa milele katika moto wa jahanama, na wenye madhambi makubwa miongoni mwa waumini pindi wanapokufa bila ya kutubia, wataingia motoni lakini hawata dumu humo na wala hatabakia motoni yeyote ambaye kwenye moyo wake kuna chembe ndogo ya Imaani isipokuwa atatolewa humo.

Imaani inakusanya itikadi ya moyo kauli na matendo, matendo ya viungo na maneno ya ulimi, atakae simamia katika njia iliyokamilika basi huyo atakuwa muumini wa kweli ambae anastahiki malipo mema na kusalimika na adhabu ya moto, kwani imaani inazidi na kkupungua, inazidi imaani kwa kufanya mambo mema na inapungua imaani kwa kutenda maasi na mambo mabaya.

Kama anavyo shuhudia muumini kuwa Muhammad (saw) ni mja wa Allah na mtume wake, mwenyezi mungu amemtumiliza kwa muongozo na dini ya haki

ili iweze kushinda dini nyingine zote, na yeye mtume ni kiumbe bora kuliko waumini wote na nafsi zao, na yeye nmi mwisho wa mitume ametumwa kwa majini na watu wote kuja kuwabashiria mema na kuwaonya kufanya shirki na mambo maovu, na alinganie kwa Allah kwa idhini yake awe ni taa yenye kuangaza, ametumwa kuirekebisha dini na dunia ili viumbe wote wasimame kwenye haki ya kumuabudu Allah peke yake asiye na mshirika na wamtake msaada katika kutafuta rizki.na watambue kuwa mwenyezi mungu anawajua zaidi viumbe wake, mwenyezi mungu ni mkweli zaidi, ana nasaha nzuri zaidi na ni mtukufu aliye wazi katika kauliamtukuze na ampende atangulize mapenzi yake juu ya kupenda viumbe wote, wamfuate katika misingi ya dini na matawi yake, waitangulize kauli yake na muongozo wake juu ya kauli na muongozo wa mtu yeyote.

Na aitakidi kuwa mwenyezi mungu amemkusanyia fadhila na mambo maalumu na ukamilifu jambo ambalo ajalifanya kwa kiume yeyote zaidi ya mtume Muhammad (saw) na mtume ni kiumbe mwenye nafasi ya juu zaidi kwa Allah, na ana cheo kikubwa zaidi, na ni mkamilifu wa fadhila kwani hakuna kheri yoyote isipokuwa aliujulisha umati wake na hakuna shari isipokuwa aliutahadharisha umati wake kutokana na shari hiyo.

Kama vile muumini aamini kila kitabu alichokiteremsha, na kila mtume aliemtuma mwenyezi mungu anayejulikana na asiyejulikana, muumini wa kweli habagui kati ya mitume na kuwaamini, kwa kuwa ujumbe wao ni mmoja nao ni kukuabudu mwenyezi mungu mmoja asiye na mshirika.

Vile vile muumini anatakiwa aamini qadar, kwani matendo yote wyafanyayo waja ya kheri au ya shari yote Allah anayajua na mwenyezi mungu kishapitisha kalamu yake, na yameshatekelezwa kwa matakwa yake na kufungamana na hikma yake Allah, Allah amewaumba viumbe wake kwa uwezo wake na matakwa yake, sio kwa matakwa yao ya kauli zao na viterndo vyao, hawakumlazimisha mwenyezi mungu kuwa awafanyie watakavyo, bali mwenyezi mungu aliwaumba kwa kutaka kwake.

Mwenyezi mungu amewachagua waumini na akawapenda kwa kuwapambia Imaani kwenye nyoyo zao, na kuwafanya wauchukie ukafiri, uovu na maasi kwa uadilifu wake na hikma yake.

Miongoni mwa misingi ya aqeeda ni pale muumini anapojipamba na dini, kwa kunasihiwa kwa ajili ya Allah, na kitabu chake na mtume wake na viongozi wa ummah na waislamu wote, muumini amrishe mema na akataze mabaya juu yay ale ambayo ni wajibu katika sharia ya uislamu, kwa kuwafanyia

wema wazazi wawili, kuunga undugu na kuwafanyia ihsani jamaa wa karibu katika familia pamoja na majirani zako wenye haki na wewe, na kuwafanyia ihsani viumbe wote, alinganie kwenye tabia njema na mazuri ya tabia njema, na akataze kulingania kati, ka mambo maovu na mabaya.

Na awe anatakidi kuwa ukamilifu wa imaani na yakini ya muumini, ni yule ambae anafanya matendo mema na kuwa na tabia njema na kuwa mkweli, na kuwaongoza watu katika njia ya kheri na kuwakataza katika njia ya shari.

Muumini wa kweli ni yule ambae anatambua kuwa jihadi katika njia ya Allah ipo inaendelea mpaka siku ya kiyama, na jihadi ndio muhimili mkuu wa dini ya kiislamu, kuna jihadi ya elimu na hoja, jihadi ya kupigana kwa silaha, nah ii jihadi ni faradhi kwa kila muislamu kuilinda dini yake kwa njia yoyote anayoweza kupigana, na kila kiongozi wa ummah anatakiwa kuitangaza awe ni kiongozi mwema au muovu aitangaze jihadi pale yatakapo timia masharti yake na sababu zake.

Na miongoni mwa misingi ya dini ya kiislamu ni kutilia umuhimu wa umoja wa kiislamu kwa kuzikurubisha nyoyo za waislamu kuwa pamoja na kuwatahadharisha na ubaya wa kutengana na kuchukiana bila ya sababu, na kuwakataza kuwaudhi

viumbe wengine kwa kumwaga damu zao, kuchukua mali zao bila ya haki na kuwavunjia heshima zao na haki zao, pia kuamrisha uadilifu katika muamiliana pamoja kati ya waislamu na waiokuwa waislamu makafiri.

Kama vile ambavyo anaitakidi muumini kuwa ummah bora ni ummah wa mtume wetu Muhammad (saw) na maswahaba bora ni maswahaba wa mtume Muhammad (saw), hasa hasa makhalifa wanne, pamoja na wale kumi walio bashiriwa pepo na mtume Muhammad (saw) na wale ahlul badri (waliopigana vita vya badri) na wale walimkubali na kumsapoti mtume katika Bai'at Ridh-wan na wale maswahaba wa mwanzo waliongia kwenye uislamu miongoni mwa Muhajirina na Answar, ni wajibu kuwapenda maswahaba wa mtume (saw) ni sehemu ya dini, na kueneza kwa kutangaza wema wao maswahaba na kunyamaza kuyatangaza yaliyosemwa katika mabaya yao.

Ni katika dini kuwaheshimu wanavyuoni na viongozi waadilifu katika watawala, na wale ambao wana nafasi za juu katika dini, na wale wenye heshima mbali mbali katika waislamu, tumuombe mwenyezi mungu awalinde na shaka, ushirikina, kuwagawa waislamu, unafiki na tabia mbaya, awathibitishe katika dini ya Mume wao mpaka siku mwisho ya mauti.

Hii ndio misingi mikuu inayofuatwa na kundi lililofaulu na misingi hii ndio inayofuatwa na wafuasi wake na kwayo wanailingania kwa watu waifuate misingi hii.

# FIHRISI YA KITABU

MISINGI YA AQEEDAH.................................................... 3

TAUHEED NA AINA ZAKE. ............................................... 3

1 : TAUHEED ALRUBUBIYYAH. ......................................... 4

2 : TAUHEED AL-ULUHIYYAH............................................ 6

3 : TAUHEED AL-ASMAAI WASWIFAAT (MAJINA YAKE ALLAH NA SIFA ZAKE)...................................................... 8

MAANA YA KALIMAT TAUHEED .................................... 10

NGUZO ZA KALIMAT LAAILAAHA ILLALLAH. .................. 11

UBORA WA KALIMAT TAUHEED ................................... 12

MASHARTI YA KALIMA YA LAAILAAHA ILLALLAH........... 14

MAANA YA KUSHUHUDIA KUWA MUHAMMAD NI MJUMBE WAKE ALLAH (SW)......................................... 23

IMAANI YA NGUZO ZAKE. ............................................ 26

1 : NGUZO YA KWANZA YA IMAAN NI KUMUAMINI ALLAH (SW)............................................................... 28

2 : NGUZO YA PILI NI KUAMINI MALAIKA WA ALLAH.... 37

3 : NGUZO YA TATU NI KUAMINI VITABU VYA ALLAH... 38

4: NGUZO YA NNE YA IMAANI NUKUAMINI MITUME WA ALLAH........................................................................ 40

5 : NGUZO YA TANO KUAMINI SIKU YA MWISHO. ........ 42

6 : NGUZO YA SITA NI QADAR........................................ 43

SHIRKI NA AINA ZAKE.................................................... 45

ITIKADI YA KUNDI LILILO FAULU. ................................... 49